# KILIMO MSETO NA URUTUBISHAJI WA SHAMBA LA MKONGE




**Imeandaliwa na**

**Kitengo cha Utafiti wa Mkonge TARI-Mlingano,**

**S.L.P 5088, TANGA.**

**Simu: +255 737 374 076**

**Barua pepe: cdmlingano@tari.go.tz**

# Utangulizi

**Kilimo mseto** ni mchanganyiko wa mazao mbalimbali na mkonge katika shamba.

Kilimo mseto katika urutubishaji udongo wa mashamba ya mkonge kina umuhimu kutokana na mfumo wa upandaji. Mfumo wa upandaji mkonge shambani una shawishi kilimo mseto ili kuboresha afya ya udongo.

## Kilimo Mseto cha Mkonge na Mahindi



## Umuhimu wa Kilimo mseto

- Kutumia ardhi kwa ufasaha.
- Kuzalisha mazao zaidi ya moja katika eneo hilo hilo na kwa gharama ndogo.
- Kupanda mazao ya jamii ya mikunde, husaidia kuongeza nitrogen ardhini na hivyo kusaidia ukuaji haraka wa mkonge.
- Mkulima hupata chakula pamoja na fedha kutokana na eneo moja.
- Humpunguzia mkulima muda na gharama za utunzaji kwa vile mazao yote yapo pamoja.
- Baadhi ya mazao hufunika ardhi na hivyo kupunguza mmomonyoko wa ardhi kwa njia ya upepo na maji ya mvua.

## Mazao yanayofaa kuchanganywa na Mkonge

Mazao yanayofaa kuchanganywa na mkonge ni maharage, fiwi, kunde, karanga, soya, choroko, alizeti,ufuta na mahindi.Aidha majani yanayofaa kwa malisho ya mifugo mfano tropical kudzu, Glycine javanica na marejea yanaweza pia kupandwa katikati ya miraba ya mikonge.

## Mazao yasiyofaa kwa kilimo mseto

- Mazao ya kudumu kama vile migomba, Minazi, Mikorosho na Michungwa yasichanganywe na Mkonge kwani kivuli cha mazao hayo huathiri Mkonge.

- Mazao kama muhogo na viazi vitamu hayafai kuchanganya na mkonge kwa sababu yanatumia rutuba nyingi ya ardhi na pia wakati wa uvunaji mizizi ilishayo mkonge inaharibiwa.

## Mambo ya kuzingatia katika kilimo mseto cha Mkonge

- Mazao yapandwe umbali usiopungua mita moja kutoka kwenye mraba wa mkonge.
- Ni muhimu katika mchanganyiko huo,mazao ya jamii ya kunde nao yawepo.
- Baada ya kuvuna mazao ya chakula mabaki yote yatawanywe shambani badala ya kuyachoma na kuyaondoa kwani ni muhimu katika kuongeza rutuba na matandazo kwenye udongo.
- Mkonge usichanganywe na mahindi,alizeti na ufuta zaidi ya misimu miwili mfululizo bali mazao ya jami ya kunde.
- Ni muhimu mazao yawekewe mbolea au mboji ya wanyama ili kurudisha virutubisho vilivyotumiwa na mazao hayo.

**Mazao yasiyoyachakula yafaayo kuchanganywa na Mkonge**



Licha ya mazao mchanganyiko kurutubisha udongo kwenye shamba la mkonge, mmea wa mkonge kwa asili yake hutunza mazingira kwani hupunguza sana mmomonyoko wa udongo

Sehemu ya ardhi kati ya nyororo za mkonge inayofaa kuchanganywa na mazao mengine.



**Sehemu mojawapo tayari imechanganywa na mahindi**





**Mimea jamii ya mikunde kunde huongeza virutubisho, huzuia magugu na kutunza unyevu nyevu shambani hivo kuboresha ukuaji wa zao la Mkonge.**

